

GRADE 4 END TERM 3 MARCH 2022

KISWAHILI

SEHEMU B

ZOEZI LA 3: KUSOMA KWA UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 5.

Msimu wa mvua ni murua sana kwa upanzi wa miti. Miti huyapa mazingira yetu sura ya kupendeza. Ule mti mdogo unaopandwa huitwa mche. Shughuli za upanzi wa miche si ya watu fulani. Ni lazima ihusishe watu wote katika jamii. Shuleni, wanafunzi wapewe miche ili kila mmoja apande angalau miche miwili. Mwanafunzi huyo ashauriwe kuitunza miche yake. Upanzi wa miche utazuia kuenea kwa jangwa. Majangwa yakienea nchini, joto huongezeka na mito kukauka. Vilevile, wanaokata miti ovyoovyo wanafaa kuchukuliwa hatua.

1. Ni msimu gani huwa murua kwa upanzi wa miti? _____
2. Tumeambiwa kuwa mti mdogo unaopandwa huitwaje?

3. Wanafunzi shuleni washauriwe kuifanyia nini miti yao midogo?

4. Je, wanaokata miti ovyoovyo wanafaa wafanyiwe nini?

5. Upanzi wa miche utazuia kuenea kwa _____

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 6 hadi la 10.

Hapo zamani za kale, mfalme Simba alikuwa mgonjwa sana, wala asiweze kukimbia kama ilivyokuwa kawaida yake. Rafiki zake wa chanda na pete, Chui na Fisi, wakamwonea huruma na kumletea vipande vya nyama ili azime njaa. Hata hivyo, vipande hivyo vya nyama havikumtoshia Simba. Maskini Simba! Alizidi kukonda na kukondeana. Siku moja, watatu hao walipokuwa pangoni mwa Simba, Simba aliwaambia, "Nimekuwa mgonjwa kwa muda sasa. Nimekuwa mnyonge zaidi. Ili nirejeshe afya yangu, nitamla mmoja wenu."

6. Wataje wanyama waliotajwa katika habari. _____

7. Simba alipoonewa huruma, aliletewa nini? _____
8. Ni nani alizidi kukonda na kukondeana? _____
9. Ili kurejesha afya yake, Simba aliamua kufanya nini?

10. Chui na fisi walimletea Simba nyama ili _____

ZOEZI LA IV: SARUFI

Piga mstari chini ya aina ya neno mabanoni

11. Nywele za Pendo zimekuwa ndefu. (kivumishi).
12. Wazee wawili walitembea polepole. (kielezi)
13. Mtoto amemwaga maji yote. (kitenzi)
14. Kalamu yangu ilipotea jana (nomino)

Andika ngeli za majina haya.

15. Joto _____
16. Chepeo _____
17. Maua _____
18. Wazazi _____

Andika sentensi upya katika wakati uliopita hali ya kuendelea

19. Mimi nitakuwa nikisoma kitabu.

20. Wageni wamekuwa wakiongea kwa sauti.

Andika katika udogo au ukubwa.

21. Jibwa _____
22. Kijito _____
23. Jitu _____
24. Kijiti _____
25. Mtoto _____

Score	
	25

